
# MAELEZO KAMILI YA CHATI YA MPANGO WA MUNGU

SOMO LA 52




*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*




# MAELEZO MAKILI YA CHATI YA MPANGO WA MUNGU

Leo tunafikia **HITIMISHO** la masomo yetu ya Biblia baada ya miezi mingi!! Tumekuwa, kwa neema ya Mungu, tukijifunza kuhusu **MPANGO WA MUNGU** katika vipengele vyake vyote kwa kina. Kama unakumbuka, **MWANZO** wa masomo yetu, ulipoona kwa mara ya kwanza **CHATI YA MPANGO WA NYAKATI**... yote yalionekana kuwa **MAPYA** na ya ajabu kwako!

**LAKINI LEO**, imekuwa **chati uliyoozoea** – ramani tukufu kwa ajili ya wanadamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu!!

NDIYO! **Biblia Iliyowekwa Katika Chati!** Tumekuwa tukijifunza vipengele vyake vyote kwa mtiririko na kuelewa kwa kina na kwa undani. Lakini leo, tutafanya jambo **tofauti!** Tutajifunza chati hii kwa **UKAMILIFU!!**

**MUHTASARI KAMILI WA CHATI YA MPANGO WA NYAKATI (A HADI Z)!!**

Sasa kuna **NJIA TATU (3)** ambazo tutazitumia kusoma na kufasiri chati hii:

1. Herufi **KUBWA** A hadi Z
2. Herufi **NDOGO** a hadi z
3. **NAMBA** 1 hadi 11

Tunahitaji kuangalia chati **KILA WAKATI** tunapojifunza somo la leo – ndiyo maana tumeiweka **juu ya ukurasa** wa somo hili. Haya, hebu tuanze na – **Herufi Kubwa A Hadi Z**.

**A**

Herufi kubwa **A**, inaashiria kipindi cha **KWANZA** cha wakati katika mpango wa Mungu –**ULIMWENGU WA KWANZA**; Hiki kilikuwa kipindi kutoka **kuumbwa kwa Adamu** hadi siku **Gharika ilipoanza**, kipindi cha miaka **1656**. Kinajulikana katika maandiko kama – *"ulimwengu ule wa zamani" – 2 Petro 3:6*.

## B

Sasa herufi kubwa **B** inaashiria kipindi cha **PILI** cha wakati katika Mpango wa Mungu – **ULIMWENGU WA PILI,** Ulianza siku Gharika ilipoanza (**B**) na unaendelea hadi siku zetu, na utahitimishwa katika kile ambacho maandiko yanakiita *"kwa moto"* – *2 Petro 3:7*. Kipindi hiki kinajulikana katika maandiko kama: *"mbingu na nchi za sasa"* (*2 Petro 3:7*), au *"ulimwengu huu wa sasa wenye uovu"* – *Wagalatia 1:4*.

## C

Herufi kubwa **C** inaashiria kipindi cha **TATU** cha wakati katika mpango wa Mungu, ambacho **HAKINA MWISHO** – **ULIMWENGU WA TATU** ; Unaanza kutoka mwisho wa miaka 6000, ambayo ilikuwa mwaka **1874**, na utaendelea **MILELE** – *"ulimwengu usio na mwisho" – Waefeso 3:21*. Kipindi hiki kinatajwa katika maandiko kama: *"mbingu mpya na nchi mpya ambayo haki yakaa ndani yake"* – *2 Petro 3:13*.

## D

HAPA tunaona kwamba kuna kipindi maalum cha **KUINGILIA** kati ya ulimwengu wa pili na wa tatu. Herufi kubwa **D** inaashiria kipindi hiki – ambacho **NDICHO TUNACHOISHI SASA!**

Herufi kubwa **D** inaashiria **ENZI YA KWANZA** kati ya **ENZI TATU** zilizomo ndani ya ulimwengu wa pili. Kipindi hiki kinaitwa –**ENZI YA MABABU(*mababu wa imani*),** Hiki kilikuwa kipindi ambacho Mungu alifanya maagano na kushughulika na watu binafsi. Walijulikana kama **"mababu"** au **"baba wa koo"**, na enzi hii ilianza baada ya gharika na **Nuhu**, ikaendelea kupitia **Ibrahimu**, **Isaka**, na kuisha na **kifo cha Yakobo mwaka 1812 K.K.**

Mwaka wa gharika kihistoria, kwa kadri tunavyokokotoa ni: **4128 – 1656 = 2472 K.K.** Hivyo basi enzi hii ilidumu kwa takribani **miaka 659** (kuanzia **2471 K.K. hadi 1812 K.K.**) (**Tunakokotoa kuanzia mwaka mmoja baada ya gharika**)

## E

Herufi kubwa **E** inaashiria **ENZI YA PILI** ndani ya ulimwengu wa pili. Kipindi hiki kinaitwa – **ENZI YA WAYAHUDI** Ilianza **na kifo cha Yakobo** na ikaendelea hadi mwisho wa *"wiki sabini"* za kibali – *Danieli 9:24*. Hii ilikuwa enzi ambapo Mungu **alitambua** na kuonyesha kibali **kwa makabila kumi na mawili** ya wana wa Yakobo **pekee**, kama tunavyosoma katika *Amosi 3:2*:

*"Ninyi peke yenu ndio niliowajua, miongoni mwa jamaa zote za dunia..."*

## F

Herufi kubwa **F** inaashiria **ENZI YA TATU** ndani ya ulimwengu wa pili. Kipindi hiki kinaitwa – **ENZI YA INJILI** Ilianza **wakati wa ubatizo wa Yesu** na itaisha na **kukamilika kwa Mwili wa Kristo**. Hii ni enzi ambapo mwito umetolewa ili **kuwaita,**

**kuwakuza, na kuwachagua** wanaounda Mwili wa Kristo – yaani wale **144,000** – *Ufunuo 14:1*.

Pamoja na mwisho wa enzi hii pia huja **MWISHO WA ULIMWENGU WA PILI**, kama tunavyoona katika mstari wa nukta-nukta kwenye chati.

## G

Herufi kubwa **G** inaashiria **ENZI YA KWANZA** ndani ya **Ulimwengu wa Tatu**. Hiki ni kipindi kiitwacho **ENZI YA MILENIA** au **ENZI YA MASIHI**. Kimeanza wakati wa **KURUDI MARA YA PILI kwa Bwana wetu mwaka 1874**, na kitaisha baada ya **kukamilika kwa miaka 1000** ya utawala Wake mwaka **2874**, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 20:4*:

*"Nao wakaishi, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu."*

Hiki ndicho kipindi cha **UTAWALA**, na pia cha **UFUFUO**, na **UREJESHO**, na **HUKUMU** ya ulimwengu – *Matendo 17:31*.

## H

Herufi kubwa **H** inaashiria kipindi cha wakati **BAADA ya kukamilika kwa Enzi ya Masihi**. Kipindi hiki kinatajwa katika **andiko moja tu** la Biblia, ambalo ni *Waefeso 2:7*:

*"Ili katika vizazi vyaja…."* (yaani: *"vizazi vijavyo"*)

Hiki ndicho kipindi ambacho kinaendelea hadi katika **UMILELE**, na ndicho kipindi ambapo **mpango wa Mungu kwa mwanadamu mkamilifu** utakuwa **ndipo unapoanza tu!!**

## I&J

Herufi **I & J** huenda zinaashiria **MUUMBA MKUU** ambaye anajulikana kama *"Mimi niko ambaye niko"* – *Kutoka 3:14*. Na **J** ni herufi ya kwanza ya jina la Baba – **YEHOVA**, na pia ya **Mwana wake wa pekee – YESU** kwa lugha ya Kiingereza. Lakini jambo hili **SI SEHEMU YA CHATI, wala SI SEHEMU YA UFASIRI wake hata kidogo!**

## K

Herufi kubwa **K -Huu ni mstari unao ashiria Asili kubwa naya juu ya MUNGU** ya kuwepo katika ulimwengu wote. Ndiyo! **UMILELE** na **ASILI YA KIMUNGU(*Divine nature*)** Ni asili ambayo, katika uumbaji wa mwanadamu, **alimiliki kiumbe mmoja tu** – yaani **MUUMBA – MUNGU BABA WA MBINGUNI mwenyewe**, kama tunavyosoma katika *1 Timotheo 6:16*: *"Aliye na kutokufa peke yake…"*

LAKINI TANGU siku ya tatu baada ya Kalvari, Mungu alimfufua Yesu pia katika **asili hii ya umilele**, kama tunavyosoma katika *Yohana 5:26*: *"Kwa kuwa kama vile Baba alivyo na uzima ndani yake mwenyewe; vivyo hivyo alimpa Mwana kuwa na uzima ndani yake mwenyewe."* Na tena katika *Ufunuo 1:18*:

*"Mimi ni yeye aliye hai; nalikuwako nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele..."*

Naam! Baada ya Yesu, Mungu sasa **ANATOA** ahadi hii *"kuu mno, ya thamani"* ya **ASILI YA KIMUNGU** kwa **KANISA LA YESU**, kama **zawadi kwa uaminifu** wao katika kufuata hatua za Yesu, kama tunavyosoma katika: *2 Petro 1:4 "Kwa njia ya hizi ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwa hizo mpate kuwa washirika wa asili ya Uungu, mkiokoka na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa." Warumi 2:7 "Wale ambao kwa saburi katika kutenda mema hutafuta utukufu na heshima na kutokufa, uzima wa milele."*

**L**

Herufi kubwa **L** inaashiria **asili ya malaika**– ambayo ni **asili ya kiroho** ya **VIUMBE WA KIROHO MBINGUNI**. Wote hawa wana **miili ya kiroho**, na kimsingi ni **WANAOKUFA** kwa asili, yaani wanaweza kufa! Bwana wetu Yesu Kristo alikuwa **WA KWANZA kuumbwa katika asili hii**. Pia **Shetani na malaika waliomuasi** nao wamo kwenye asili hii ya kuwepo, na hivyo wote **wataangamizwa**.

Rejea *Mathayo 25:41, 46 – "moto wa milele"*, au pia *"adhabu ya milele"*, ambayo humaanisha **MAUTI YA MILELE**.

Asili hii ya kuwepo ni **YA JUU ZAIDI** kuliko ile ya **ASILI YA UBINADAMU MKAMILIFU**, kama tunavyosoma katika *Zaburi 8:5*: *"Umemfanya mdogo punde kuliko malaika..."*

**M**

Herufi kubwa **M** inaashiria **asili** ambayo ni **ya kipekee** kwa **Enzi ya Injili pekee**. Hii ni asili ya **KUZALIWA KIROHO (Spirit begatal)** kwa wale **WAKRISTO WALIOJITOA** ambao hutoa miili yao kuwa *"dhabihu iliyo hai"*, kama inavyoelezwa katika:

*Warumi 12:1 "Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana."* ...na kuwa **VIUMBE VIPYA**, kama tunavyosoma katika: *2 Wakorintho 5:17 "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya."*

Wao hupitia **MAENDELEO WAKIWA KATIKA MWILI**, kupitia mateso, kwa sababu wanatafuta kuishi kwa **HAKI** katika ulimwengu uliojaa uovu, kama tunavyosoma katika: *2 Timotheo 3:12 "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa."*

Naam! Wakristo hawa walio **"viumbe vipya"**, **BAADA YA KIFO**, na katika **ufufuo**, **huzaliwa kwa Roho** – yaani, huwa **VIUMBE WA KIROHO** – *Yohana 3:8*.

**Viumbe vipya** watapata **asili MBILI** za uhai wa kiroho. Kundi la **"kundi dogo"** hupokea **asili ya Kimungu isiyokufa**, na **"mkutano mkuu"** hupokea **asili ya malaika ambayo ni ya kufa**.

**N**

Herufi kubwa **N** ni mstari unaonesha asili ya **mwanadamu katika ukamilifu, au mwanadamu aliyehesabiwa haki.** Katika msitari huu waliwahi kuwepo **watu wawili tu waliokuwa wakamilifu**: **Adamu** na... **"mtu" Kristo Yesu!!**

Mstari huu unamaanisha asili ya **miili ya nyama iliyokamilika**, lakini ni **ya kufa kwa asili**, ikimaanisha kwamba kutenda dhambi husababisha **hukumu ya mauti**, kama ilivyoonekana katika maisha ya mtu wa kwanza mkamilifu – Adamu.

Hii ndiyo **asili** ambayo **wanadamu wote** watapata **nafasi ya kuifikia... na kuipokea** wakati wa **Enzi ya Milenia**.

Herufi kubwa **O** haijumuishwi katika chati hii.

# P

Herufi kubwa **P** inaashiria **asili ya kipekee ya kuwepo**, ambayo ilikuwapo tu katika **Enzi ya Wayahudi**. Ni hali ya kiibada iitwayo **hali ya kuhesabiwa haki kwa mfano iliyokuwa katika taifa la Israeli pekee.**

Hali hii ilifikiwa kupitia sadaka za kila mwaka za **Siku ya Upatanisho**, kama tunavyosoma katika *Mambo ya Walawi 16:30, 34*:*"Maana siku hiyo atafanya upatanisho kwa ajili yenu, ili kuwatakasa, ili mpate kutakasika na dhambi zenu zote mbele za Bwana... Nayo itakuwa amri ya milele kwenu, ili kuwafanyia upatanisho wana wa Israeli kwa ajili ya dhambi zao zote, mara moja kila mwaka."*

Sadaka hizi ziliwafanya waonekane kuwa **safi kwa mfano (kifano)** mbele za Bwana. Kwa hiyo, hali hii iliwaweka katika **kiwango cha juu** kuliko ulimwengu kwa ujumla, kama inavyoonyeshwa katika chati – lakini kwa sababu **hawakuwa wakamilifu kweli**, wala **hawakuwa bila dhambi**, ngazi hii ya **P** ni **chini** ya ile ya binadamu mkamilifu ya msistari wa **N**.

Herufi kubwa **Q** pia haipo katika chati hii.

# R

Herufi kubwa **R** inaashiria **Asili ya kuwepo** ambayo **ULIMWENGU WOTE WA WANADAMU** umeishi tangu **anguko katika bustani ya Edeni**. Ni hali ya – **KUANGUKA, UOZO WA DHAMBI NA MAUTI** Hali hii inahusisha **mwili unaokufa**, unaoanza kufa **tumboni**, na kumalizika **kaburini!!**

Hakuna **uzima** wala **haki ya kuishi** katika hali hii ya kuwepo. Ni hali ya **kifo** mbele za Mungu, na kwa sababu hiyo Yesu aliwataja wanadamu wote kuwa wamo katika hali hiyo, kama tunavyosoma katika *Luka 9:60*: *"Yesu akamwambia, Waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe uende ukahubiri ufalme wa Mungu."*

# S

Herufi kubwa **S** inaashiria kipindi cha wakati baada ya **Kurudi kwa Bwana wetu Yesu Kristo mwaka 1874**. Kipindi hiki kinaitwa – **Kipindi Cha Mavuno Cha Enzi Ya Injili Na... Pia Kipindi Cha "Wakati Wa Taabu"** Ni kipindi kinachoanza hapa (**S**) na kinaendelea hadi **kukamilika kwa kanisa** na **"kuungua kwa magugu"** kama tunavyosoma katika *Mathayo 13:30* – katika **"wakati wa taabu kuu"** ambao **utahitimisha enzi** na pia **ulimwengu wa pili**.

Hili hutokea katika **kipindi cha kipekee cha KUINGILIA** kati ya **ulimwengu wa pili na wa tatu**.

Katika kipindi hiki, **uteuzi wa mtu mmoja mmoja wa Kanisa** unakamilika... na **mifumo ya uongo ya kidini (ya jina tu)** inahukumiwa na kuangamizwa. Katika kipindi hiki pia, taifa la kale

la **ISRAELI linarejeshwa katika kibali**, na linakawa taifa tena mnamo – **14 Mei 1948!!**

Herufi kubwa **T, U na V** hazijumuishwi katika chati hii.

## W

Herufi kubwa **W** inaashiria hali ya ulimwengu wa wanadamu **BAADA YA UFALME KUONEKANA WAZI** katika Israeli. Hii ni hali ya – **Ulimwengu Kupandishwa Hadi Ukamilifu Wa Kibinadamu... Na Uzima** Hii hufikiwa **polepole** kupitia hali na njia ya maisha iitwayo – **NJIA YA KUU**(*Isaia 35:8*)

Katika kipindi hiki, ulimwengu wa wanadamu **wanaorudi kutoka kaburini**, na kutoka katika hali ya "kifo"... **macho na masikio yao ya kuelewa** hufunguliwa, kama tunavyosoma katika: *Isaia 29:18 "Na siku hiyo viziwi watasikia maneno ya kitabu, na macho ya vipofu yataona toka gizani, na toka utusitusi."* ...na **polepole huanza kujifunza njia za haki**, kama tunavyosoma katika: *Isaia 26:9 "Kwa roho yangu nimekutamani usiku; naam, kwa roho yangu iliyo ndani yangu nitakutafuta mapema; kwa maana hukumu zako zikiwa katika nchi, wakaao duniani hujifunza haki.*

Naam! **Watapewa wote** fursa ya ajabu ya **KURUDI KATIKA UKAMILIFU WA UBINADAMU** na uzima, kama tunavyosoma katika *Ayubu 33:25*: *"Mwili wake utakuwa na afya kuliko wa mtoto; atarudi katika siku za ujana wake."*

Ndiyo! Huu Ndio **Wokovu Mkuu Na Wa Ajabu** Ambao Mungu Ameuanda Kwa Ajili Ya Wanadamu Wote!!

Kisha, **ulimwengu wa wanadamu waliokamilishwa** wakati huo **utafanyiwa mtihani wa uaminifu wao na tabia yao**, wakati **mwishoni mwa Enzi ya Milenia**, Shetani – ambaye alikuwa

amefungwa hadi wakati huo – ataachiliwa kama tunavyosoma katika *Ufunuo 20:7–9*: *"Na ile miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa katika kifungo chake. Naye atatoka kwenda kuwadanganya mataifa walioko katika miisho minne ya dunia, Gogu na Magogu, kuwakusanya kwa vita; hesabu yao ni kama mchanga wa bahari. Wakapanda juu katika nchi yote, wakazunguka kambi ya watakatifu na mji ule wa kupendwa; moto ukashuka kutoka mbinguni kwa Mungu, ukawala."*

Naam! Baada ya **HUKUMU HII YA MWISHO**, Shetani na wale waliomo katika mfano wake **wataangamizwa** katika **mauti ya pili**, na jamii ya wanadamu waliokamilika na waaminifu **watairithi dunia** kama tunavyosoma katika *Mathayo 25:34*: *"Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu."* ...kama **WAFALME**, kila mmoja wao, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 22:5*: *"Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawahitaji taa, wala nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwapa nuru, nao watamiliki milele na milele."*

Herufi kubwa **X, Y, na Z** hazijumuishwi katika chati hii.

Baada ya kutazama **HERUFI KUBWA**, sasa tuangalie – **herufi ndogo a hadi z**

## a

Herufi ndogo **a** inaashiria **umbaji wa kwanza wa mwanadamu kutoka kwa Mungu** – yaani **ADAMU**. Aliumbwa *"kwa mfano... na... sura"* ya Mungu kama tunavyosoma katika *Mwanzo 1:26*: *"Kisha Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila kitambaacho juu ya nchi."*

Naam! Aliumbwa akiwa **MKAMILIFU**, akiwa na **uzima** na **haki ya kuishi!!** Kisha baadaye, kwa ajili ya **"msaidizi wa kufanana naye"** (*Mwanzo 2:18*), Mungu alimuumba mwanamke **HAWA** kutoka kwa **ubavu wa Adamu**, kama tunavyosoma katika *Mwanzo 2:22*: *"Na ule ubavu, alioutoa katika Adamu, Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu."*

Naam! Naye pia aliumbwa akiwa **MKAMILIFU** – lakini **alikuja kutoka ndani ya Adamu**! Adamu pia alikuwa **KICHWA** na **BABA wa familia yote ya wanadamu**, kama tunavyosoma katika *Matendo 17:26*: *"Naye amefanya kila taifa la wanadamu, kutoka katika mtu mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote…"*

## b

Herufi ndogo **b** inaashiria **ULIMWENGU WA WANADAMU katika Ulimwengu wa Kwanza**. Wote **walirithi dhambi na mauti** kutoka kwa Baba yao Adamu na Mama yao Hawa, na **wamezaliwa katika hali hiyo**, kama tunavyosoma katika *Zaburi 51:5*:

*"Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; Mama yangu alinichukua mimba hatiani."* Hali hii ya kuishi katika **hali ya dhambi na mauti** inaitwa – **NJIA PANANA** (*Mathayo 7:13*).

Na matokeo yake ni kwamba, katika Ulimwengu wa Kwanza, **jamii nzima ya wanadamu ilizaliwa katika dhambi na mauti**. Watu hawa hasa walizama katika maovu chini ya **mvuto wa malaika waliochanganyika na binadamu** na kuzaa kizazi kipya kilichoitwa... **WANEFILIMU** *(Biblia ya NIV)*, kama tunavyosoma katika *Mwanzo 6:4*:

*"Nako kulikuwa na majitu duniani siku zile; tena baadaye, wana wa Mungu walipoingia kwa binti za binadamu, wakazalia wana; hao ndio waliokuwa hodari zamani, watu wenye sifa."*


Naam! Hiki **kizazi kipya cha mchanganyiko wa malaika na binadamu** kiliwaongoza wanadamu katika **aina zote za uovu**, kama tunavyosoma katika *Mwanzo 6:5*: *"Bwana akaona ya kuwa uovu wa mwanadamu ni mwingi duniani, na ya kuwa kila kusudi la mawazo ya moyo wake ni mbaya tu siku zote."* Hivyo Mungu alileta **GHARIKA** na kuangamiza ule **"ulimwengu wa zamani..."** *– 2 Petro 3:6*

**c**

Herufi ndogo **c** inaashiria "Baba wa Imani" – yaani **ABRAHAMU**. Alionyesha **IMANI KUBWA** kwa Mungu kiasi cha kuwa tayari kumtii Mungu na kumtoa sadaka mwanawe mpendwa na wa pekee – **Isaka**, kama tunavyosoma katika *Mwanzo 22:12*: *"Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno lo lote; kwa kuwa sasa najua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukumzuilia mwanao, mwanao wa pekee, usimtoe kwangu."* Naam! Aliitwa *rafiki wa Mungu* na alihesabiwa kuwa mwenye haki kwa sababu ya imani yake kama tunavyosoma katika *Isaya 41:8*: *"Lakini wewe, Israeli, u mtumishi wangu,*

*Yakobo niliyekuchagua, mzao wa rafiki yangu Ibrahimu."* Na tena katika *Yakobo 2:23*: *"Na maandiko yakatimizwa yasemayo, Ibrahimu alimwamini Mungu, hilo likahesabiwa kuwa haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu."*

Ingawa hakuwa mkamilifu wala hana dhambi, tunamwonyesha hapa kama **aliyehesabiwa haki**, hata kabla ya taifa la israeli kuundwa na siku yao ya upatanisho kuanzishwa – kwa maana **mungu alihesabu imani yake kuwa haki**. Yeye ni **mtu wa kipekee sana kwa mungu**, na kwake alipewa kile tunachokiita leo hii kuwa ni **"ahadi ya ibrahimu"** (*mwanzo 22:16–18*), ambayo ni ahadi ya **ukombozi wa baadaye na baraka kwa ulimwengu wote wa wanadamu** kupitia uzao wake.




Herufi ndogo **d** inaashiria **ulimwengu wa wanadamu katika hali ya kuanguka dhambi katika ulimwengu wa pili**. Naam! Uzao baada ya gharika ulianza tena kupitia watoto watatu wa Nuhu – **YAFETHI, SHEMU na HAMU**, kama tunavyosoma katika *Mwanzo 9:18–19*: *"Na wana wa Nuhu waliotoka katika safina walikuwa Shemu, na Hamu, na Yafethi; naye Hamu ndiye baba yake Kanaani. Hawa watatu ndio wana wa Nuhu; na kwa hao dunia yote ikajaa watu."*

Naam! **Makabila yote ya sasa** yalitokana na watoto hao wa Nuhu – **Yafethi** alikuwa baba wa **kabila jeupe la Ulaya (Wazungu)**, **Shemu** akawa baba wa **mataifa ya Kiasia**, na **Hamu** akawa baba wa **kabila la watu weusi (Waafrika)**. Huu pia ulikuwa ulimwengu uliotokana katika **hali ya dhambi na mauti**. **NJIA PANANA** iliendelea kuwa **njia pekee** hadi **kifo cha Yesu**.

## e

Herufi ndogo **e** inaashiria **hali ya kuhesabiwa haki kwa njia ya mfano kwa israeli kama taifa**. Hii ilikuwa katika kipindi kiitwacho **ENZI YA WAYAHUDI**, ambapo kwa kupitia *sadaka za mafahali na mbuzi* katika **Siku yao ya upatanisho ya kila mwaka**, walipokea **kuhesabiwa haki kwa mfano** kutoka kwa Mungu kwa ajili ya dhambi zao. Hii pia ilikuwa enzi ambayo Mungu **aliwapendelea Waisraeli** kuliko mataifa yote, kama tunavyosoma katika *Amosi 3:2*: *"Ninyi peke yenu ndiyo niliowajua, miongoni mwa jamaa zote za dunia..."*

Naam! Israeli walibarikiwa chini ya **agano la sheria**, na walipokea baraka nyingi – na labda kubwa zaidi ya zote ilikuwa **kuzaliwa kwa mwana wa mungu** kama Myahudi, kama tunavyosoma katika *Warumi 9:4–5*: *"Ambao ni Waisraeli; waliofunguliwa kuwa wana, na huo utukufu, na maagano, na kupewa sheria, na ibada ya Mungu, na ahadi zake; ambao mababu ni wao, na katika hao alitoka Kristo kwa jinsi ya mwili; naye ni juu ya vitu vyote, Mungu, mwenye kubarikiwa milele. Amina."*

## f

Herufi ndogo **f** inaashiria **kipindi cha wakati baada ya Yesu kubatizwa na kutiwa mafuta**, mwishoni mwa Enzi ya Wayahudi, kiitwacho **kipindi cha mavuno cha enzi ya wayahudi**. Hiki ndicho kipindi ambacho **"ngano" ilitenganishwa na "makapi"**, kama tunavyosoma katika *Mathayo 3:12*: *"Yeye anao upepo mkononi mwake, naye ataisafisha sakafu yake kabisa, na kuikusanya ngano yake ghalani; bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika."*

Hii, bila shaka, **iliashiria kutenganishwa kwa Wayahudi wa kweli na wa jina tu**. Hiki pia ndicho kipindi ambapo **nyumba ya israeli ya jina tu ilikataliwa**, kama tunavyosoma katika *Mathayo 23:38*: *"Tazama, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa."*

Na **mwisho wa kipindi hiki**, taifa lenyewe **liliharibiwa mwaka 70 B.K.**, jambo ambalo lilikuwa ni **utimilifu wa unabii** uliorekodiwa katika *Danieli 9:26*: *"Na baada ya majuma sitini na mawili Masiya atakatiliwa mbali, lakini si kwa ajili yake mwenyewe; na watu wa mkuu atakayekuja wataharibu mji na patakatifu; na mwisho wake utakuwa kama kwa gharika, na hata mwisho wa vita kutakuwa na ukiwa uliokusudiwa."*

**Kundi la "ngano"** kutoka mavuno haya lilikuja kuwa **wanachama wa kwanza wa kanisa la yesu kristo**.

**g**

Herufi ndogo **g** inaashiria **bwana wetu yesu kristo wakati wa ubatizo wake**. Ni katika ubatizo wake ambapo Bwana alipokea **UPAKO wa Roho Mtakatifu** (*Mathayo 3:16*), na pia **alizaliwa kwa roho** na kuwa **kiumbe kipya**. Kabla ya hapo alikuwa **MTU MKAMILIFU**, na herufi **g** hapa inaashiria hasa **"mtu Kristo Yesu"** wakati wa ubatizo wake akiwa na umri wa miaka 30, kama tunavyosoma katika *Luka 3:22–23*: *"Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili kama hua; na sauti ikasikika kutoka mbinguni, Ikisema, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimeridhika nawe. Na Yesu mwenyewe alipokuwa aanza kazi yake, alikuwa mtu wa miaka kama thelathini, naye alikuwa, kana kwamba, mwana wa Yusufu…"*

## h

Herufi ndogo **h** inaashiria **yesu kama kiumbe kipya**, aliyezaliwa kwa Roho, na kila siku **akiutoa mwili wake kama "dhabihu iliyo hai"**, akifanya mapenzi ya Baba yake katika kipindi cha **miaka 3½ ya huduma yake**, kuanzia mwaka **29 B.K. hadi 33 B.K.**

## i

Herufi ndogo **i** inaashiria **yesu katika hali ya roho na uwepo wake baada ya kufufuka** siku ya tatu. Alikuwepo katika hali hii kwa kipindi cha **siku 40 duniani**, kama tunavyosoma katika *Matendo 1:3*: *"Ambaye aliwajionyesha kuwa hai baada ya kuteswa kwake, kwa vielelezo vingi visivyoweza kushindwa, akionekana kwao siku arobaini, na kusema mambo yanayohusu ufalme wa Mungu."* Naam! Ni katika kipindi hiki ambapo alijionyesha kwa mitume na wanafunzi **mara 11**, kwa muda mfupi, ili kuthibitisha kuwa **yuko hai na amefufuka**. BAADA ya siku hizo 40 **alipaa mbinguni**, kama tunavyosoma katika *Matendo 1:9*: *"Alipokwisha kusema hayo, alipokuwa akitazama, akachukuliwa juu; wingu likampokea machoni pao."*

Herufi ndogo **j** haijumuishwi katika chati hii.

## k

Herufi ndogo **k** inaashiria **Yesu katika utukufu wa asili ya mungu**. Hii ilikuwa ni **UTIMILIFU** wa lile lililotabiriwa katika *Yohana 5:26*:

*"…kama vile Baba alivyo na uzima ndani yake mwenyewe; vivyo hivyo alimpa Mwana kuwa na uzima ndani yake mwenyewe."* Hata andiko la *1 Timotheo 6:16* linamhusu **YESU** katika **Asili ya Kimungu ya kutokufa**, kwa kuwa wakati Mtume Paulo aliandika barua hiyo kwa Timotheo, **YESU PIA alikuwa katika asili hiyo ya Kimungu**. Hivyo, kwa kutumia maneno *"yeye peke yake mwenye kutokufa…"*, ni wazi kuwa **mtu pekee anayezungumziwa hapa kuwa na asili hiyo ya kutokufa ni Yesu**, ingawa ukweli unabaki kuwa **Mungu naye yumo katika asili hiyo hiyo**. Lakini **hapaswi kufananishwa** na viumbe vyake vingine, hata kama viko katika kiwango hicho, kwa kuwa katika mafananisho yote *"YEYE ANATENGWA"*, kama tunavyosoma waziwazi katika *1 Wakorintho 15:27*: *"Maana amevitia vitu vyote chini ya miguu yake. Lakini asemapo, Vitu vyote vimewekwa chini yake, ni dhahiri ya kuwa yeye aliyemwekea vitu vyote chini yake, amehesabiwa kuwa si mmojawapo wao."* Naam! Kwa kuwa **ni kwake kunahusiana na ukuu wa MUUMBA**, ambaye **HAFANANISHWI** na kiumbe chochote! Ambaye juu yake Mtume Paulo aliandika katika *Matendo 17:28*: *"Kwa maana ndani yake twaishi, na kusonga, na kuwapo kwetu; vile vile kama baadhi ya washairi wenu walivyosema, Kwa maana sisi sote tu wazao wake."*

## I

Herufi ndogo **I** inaashiria **yesu kama kichwa kisichoonekana cha kanisa katika enzi ya injili**. Naam! Katika kipindi chote cha Enzi ya Injili, Bwana amekuwa **MWAMINIFU kwa maneno yake** katika *Mathayo 28:20*: *"Nami nipo pamoja nanyi siku zote…"* Kama **KICHWA cha kanisa** (*Waefeso 1:22*), amekuwa **akilisimamia kanisa** kutoka mbinguni kama tunavyosoma katika *Ufunuo 1:13*: *"Na katikati ya vile vinara saba vya taa alikuwako mmoja aliyefanana na Mwana wa Adamu, aliyevikwa vazi refu, na kujifunga kifuani na mshipi wa dhahabu."* Naam! Anaketi **"mkono wa kuume wa Ukuu wa Juu"** (*Waebrania 1:3*). Hili **kiongozi wake asiyeonekana** limepelekea **wengi kudai uongozi wa**

**kuonekana**, jambo ambalo Yeye mwenyewe alilitabiri katika *Yohana 5:43*: *"Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, wala hamnipokei; mwingine atakuja kwa jina lake mwenyewe, huyo mtampokea."* Na tena katika *Mathayo 24:5*: *"Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ndiye Kristo; nao watadanganya wengi."* Naam! Hii ni rejea ya Bwana kwa **mifumo ya kanisa ya MPINGA KRISTO!**

**m**

Herufi ndogo **m** inaashiria **KUNDI KUBWA** kati ya yale makundi mawili yaliyoko katika *"msitari wa asili ya kuzaliwa kwa roho"* – ni kundi la **wanawali wajinga**, au kwa kivuli cha Hema ya Kukutania – **kundi la mbuzi wa azazeli**. Hili ni kundi la *"viumbe vipya"* ambao **hawafikii ukamilifu wa "mfano wa Mwana"**, na **hawatimizi kwa hiari kile walichokubaliana kwa agano** – yaani kujitoa kikamilifu. Tunalisoma hili kwa uwazi katika *Luka 14:33*: *"Kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu."* Naam! Kuna **wakristo wengi** wa kundi hili toka siku ya Pentekoste hadi leo, lakini **idadi kubwa zaidi ya kundi hili itakuwepo baada ya kukamilika kwa Mwili wa Kristo**. Wote hawa **walishindwa kukimbia kwa bidii ili wapate tuzo**, kama tunavyosoma katika *1 Wakorintho 9:24*: *"Hamjui ya kuwa wale washindanao katika machezo hukimbia wote, lakini mmoja hupata tuzo? Basi, kimbieni namna hiyo ili mpate."*

**n**

Herufi ndogo **n** inaashiria **KUNDI DOGO** kati ya yale mawili yaliyoko katika *"msitari wa asili ya kuzaliwa kwa roho"* – ni kundi la **WANAWALI WENYE HEKIMA**. Bwana wetu aliita kundi hili *"kundi*

*dogo"* katika *Luka 12:32*: *"Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme."* Naam! Hawa ndio **wafuasi wa hatua zake**. Wameelezwa kuwa *"humfuata Mwana-Kondoo kila aendapo"* kama tunavyosoma katika *Ufunuo 14:4*: *"…Hao ndio wafuatao Mwana-Kondoo kila aendapo. Hao walinunuliwa kutoka kwa wanadamu, kuwa malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo."* Hawa ndio **WAAMINIFU** kwa *agano lao la kujitoa sadaka*, na kwa hivyo huitwa *"waliitwa, walioteuliwa na waaminifu"*. Kwa pamoja, **m** na **n** huunda **KUNDI LA WALIOCHAGULIWA** katika kanisa la Yesu Kristo.

Herufi ndogo **o** haijumuishwi katika chati hii.

**p**

Herufi ndogo **p** inaashiria **kundi la kwanza** katika kanisa la Yesu Kristo – yaani kundi la **"WALIOITWA"** au **WAAMINIO**. Hawa ni wale walio katika kila dhehebu ambao **wanamwamini Yesu Kristo**, lakini **hawajamfuata** katika kujitoa sadaka binafsi. Kundi hili linaonyeshwa katika *vivuli vya Hema ya Kukutania* kama **Walawi,** ambao **walikuwa katika "ua wa nje" daima**. Naam! Wakristo hawa **wanaamini kwa Bwana**, huanza **kusoma Biblia**, na hujaribu **kuishi kwa maadili mema** – jambo hili linawakilishwa na *kuosha mikono na miguu kwenye birika la shaba*. Hili ndilo kundi ambalo Mtume Paulo analihutubia katika *Warumi 12:1*: *"Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana."* Naam! Hapa neno *"ndugu"* linaelekezwa kwa wale ambao tayari ni *"waaminio"* kwa Bwana. Lakini **wachache tu wa kundi hili hutii**, kama Yesu alivyosema: *"Wengi wameitwa, lakini wachache wamechaguliwa"* – *Mathayo 22:14*.

Naam! **Waamini wachache tu** huendelea mbele na kuwa **wafuasi wa kweli**! Kundi hili la *waamini tu* halina **urithi wa mbinguni**, kwa sababu **hawajazaliwa kwa roho**, na kwa hiyo **si viumbe vipya**, jambo ambalo ndilo **sharti kuu** la kupata uzima wa mbinguni, kama Yesu alivyosema wazi katika *Yohana 3:3*: *"Yesu akajibu, Amini, amini, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu."* Hawa wako katika **hali ya kuhesabiwa haki ya muda** kulingana na **imani yao kwa Yesu** kama tunavyosoma katika *Warumi 5:1*: *"Basi kwa kuwa tumehesabiwa haki itokayo kwa imani, na tuwe na amani kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."*

**q**

Herufi ndogo **q** inaashiria **KUNDI MAALUMU katika kanisa** ambalo linajumuisha **wafiki na wasioamini**. Kundi hili kwa jina tu hujifanya kuwa ni Wakristo, kwa sababu **wamezaliwa katika familia za Kikristo**, lakini **hawana imani**, wala **hawamwamini Yesu wala kazi yake ya ukombozi msalabani**. Kwao, msalaba na ujumbe wake ni *"upumbavu"*, kama tunavyosoma katika *1 Wakorintho 1:18*: *"Maana neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu."* Hawa hata **hawawezi kuhesabiwa haki**, kwa kuwa **hawana imani hata kidogo!** Miongoni mwa kundi hili wamo **wachungaji na wahubiri wengi** ambao *"huuza Neno la Mungu kwa faida"*, kama tunavyosoma katika *2 Wakorintho 2:17*: *"Kwa maana sisi si kama wengi, watiao changanyiko neno la Mungu..."* (Katika tafsiri ya *NIV* ni: *"sisi hatuiuzi neno la Mungu kwa faida"*).

Naam! Katika dunia ya leo ya kisasa iliyojaa **sayansi** na **ukosoaji wa juu wa Maandiko**, kundi hili ndani ya makanisa **limeendelea kuongezeka sana!!**

A

Herufi ndogo **r** inaashiria **kurudi mara ya pili kwa bwana wetu**. Maandiko yanatufundisha kuwa kurudi huku ni **KABISA KUSIKOONEKANA kwa jicho la mwili**, na hutambulikana tu kwa **macho ya imani** au *"macho ya ufahamu"*, kwani uwepo wake wa awali unaanza kama *"mwizi ajaye usiku"*, kama tunavyosoma waziwazi katika *1 Wathesalonike 5:2*: *"Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana huja kama vile mwivi ajavyo usiku."*

Naam! Hili linatufunulia kwa **lugha ya mfano** jinsi uwepo wa pili wa Bwana **utakavyokuwa wa siri na usiojulikana!** Kwa kuwa yeye ni *"Mungu Mkuu"* (*Isaya 9:6*) katika **Asili ya Kimungu**, uwepo wake wa pili umegawanyika katika **hatua tatu**: *Parousia, Epifania*, Na *Ufunuo (Apokalupsis)*. Uwepo huu ulianza **Oktoba 1874** na utaendelea hadi **2874**, ambapo maneno ya *Ufunuo 1:7* yatakuwa yametimia: *"Tazama, anakuja na mawingu; na kila jicho litamwona…"*

Njia nyingine ya kufasiri herufi **r** ni kuwa pia inawakilisha kundi la *"**waliokufa katika kristo**"… WANAOFUFUKA KWANZA*. Hili ni kundi kutoka *Mwili wa Kristo* kama tunavyosoma katika *1 Wathesalonike 4:16*: *"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, pamoja na sauti ya malaika mkuu, na pamoja na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza."*

Naam! Sehemu hii ya **MWILI WA UTUKUFU** ni wale waliolala toka Pentekoste hadi **Aprili 1878**. Ufufuo wa kundi hili unaonekana tena katika *1 Wakorintho 15:52*: *"Katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, nao wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu…"* Idadi yao **SIYO 144,000 wote**, bali ni **SEHEMU TU** ya idadi hiyo. Miongoni mwa kundi hili walikuwemo **MITUME KUMI NA WAWILI**, na **WATUMISHI SITA**

**kati ya wale saba waliotajwa kama "malaika wa Bwana"** (*Ufunuo 1:20*).

Sababu ya kutafsiri herufi **r** kuwa inawakilisha **YESU katika kurudi kwake mara ya pili**, na pia **SEHEMU YA MWILI WAKE iliyofufuliwa kwanza mwaka 1878**, inapatikana katika *Yohana 14:3*: *"Nami nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena na kuwapokea kwangu;…"* Naam! Wao wanakuwa **SEHEMU YA Mwili Wa Utukufu Wa Kristo**, na wanahesabiwa pamoja na Yesu katika kazi ya **HUKUMU, UREJESHO, na UTAWALA**. Sifa hii ya **UMOJA WA MWILI MMOJA** imeelezwa kwa uzuri katika *1 Wathesalonike 4:17*: *"…na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele."*

**s**

Herufi ndogo **s** inaashiria **WANACHAMA WA "KUNDI DOGO"… WANAOTENGANISHWA NA BABELI**. Hili linafanyika katika **KIPINDI CHA MAVUNO** cha Enzi ya Injili baada ya mwaka **1874**. Kundi hili pia linawakilisha **sehemu ya Mwili wa Kristo** inayojulikana kama: *"…sisi tulio hai, tuliosalia"*, kama tunavyosoma katika *1 Wathesalonike 4:17*: *"Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu..."*

Kuhusu kundi hili, Mtume Paulo anasema **"hawatalala wote,"** bali **katika muda wa kufumba jicho tu watabadilishwa**, kama tunavyosoma katika *1 Wakorintho 15:51*: *"Sikilizeni, nawaambieni neno la siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika,"*.

Je, hii inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba kwa kundi hili la *"MWILI"*, **wakati wa kifo ni wakati wa ajabu**, kwa kuwa *"kwa kufumba na kufumbua jicho"*, hupokea **UFUFUO WA KWANZA**, kama tunavyosoma katika *1 Wakorintho 15:54*: *"Lakini huu uharibikao*

*utakapovikwa kutoharibika, na huu wa kufa utakapovikwa kutokufa, ndipo litakapotimia neno lililoandikwa…"*

Naam! Kundi hili ndilo linatajwa kwa hakika katika *Ufunuo 14:13*: *"Nikaisikia sauti kutoka mbinguni ikiniambia, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapumzike katika kazi zao; maana matendo yao yafuatana nao."*

Neno *"tangu sasa"* linawakilisha kipindi **baada ya mwaka 1878**. Kwa maana **ufufuo wa kwanza** umekuwa **katika mchakato** tangu **Aprili 1878**. Kundi hili pia linajulikana kama **"watakatifu wa kundi la miguu"**, ambao wametajwa katika *Isaya 52:7*: *"Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima miguu yake aletaye habari njema, atangazaye amani; yeye aletaye habari njema ya mema, atangazaye wokovu, amwambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki!"* Tena katika *1 Samweli 2:9*: *"Atawalinda miguu ya watauwa wake, bali waovu watanyamazishwa gizani; maana kwa nguvu hakuna mtu atakayeshinda."* Naam! Hawa ndio **wamebarikiwa** kuwa sehemu ya Mwili wa Kristo ambao **walibaki katika mwili** hata baada ya na wakati wa **kurudi kwa pili kwa Bwana**.

**t**

Herufi ndogo **t** inaashiria **kundi la Wakristo waliotoa maisha yao wakfu** lakini **walibaki baada ya kukamilika kwa Mwili wa Kristo**. Hili ni **KUNDI KUBWA (Great Multitude)**. Hali ya kiakili ya kundi hili inaelezwa kinabii katika *Yeremia 8:20*: *"Mavuno yamepita, kiangazi kimekwisha, wala sisi hatujaokolewa."* Naam! Hawa huingia katika **DHIKI KUU** wakati wa *"wakati wa taabu kuu wa ulimwengu"*, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 7:14*: *"Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hawa ndio waliotoka katika dhiki kuu, wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo."*

Kisha hutoa **ushuhuda mkubwa kwa Mungu na kwa Ufalme**, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 19:6*: *"Nikasikia kama sauti ya mkutano mkubwa wa watu, na kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi kubwa, ikisema, Haleluya! Kwa kuwa Bwana Mungu wetu Mwenyezi anamiliki."* Hapo ndipo wanapopokea **ufufuo wa pili**, kwa kuwa wao *"huwafuata"* Mwili wa Kristo au *"Bibi-arusi"* wa Kristo hadi mbinguni, kama ilivyoelezwa kinabii katika *Zaburi 45:14*: *"Ataletwa kwa mfalme katika mavazi ya kazi ya chelezo; wanawali wenzake wanaomfuata wataletwa kwako."*

**u&v**

Herufi ndogo **u** na **v** zinawakilisha **MIFUMO YA MAKANISA kwa namna ya Jina (Nominal Church Systems) KATIKA HUKUMU**. Mifumo hii ya makanisa ya jina na wanachama wake – yaani **waaminio wa jina tu (u)** na **wanafiki (v)** – kama mifumo, **inaharibiwa**, na **imani zao za uongo na mafundisho yao hufichuliwa** wakati wa *"taabu kuu"* itakayowajia, kama tunavyosoma katika *1 Wakorintho 3:12*: *"Lakini mtu akijenga juu ya msingi huu dhahabu, fedha, mawe ya thamani, miti, majani, nyasi,"* Maneno *"miti, majani, nyasi"* yanawakilisha **uongo**, kinyume na *"dhahabu, fedha, mawe ya thamani"* ambayo yanawakilisha **kweli**.

Mifumo hii inaitwa katika Maandiko kuwa ni *"Babeli"* – ikimaanisha **machafuko ya mafundisho**. Hii ndiyo **MIFUMO YA MPINGA KRISTO** ambayo itaangamizwa katika **kipindi baada ya kurudi kwa pili kwa Bwana**, kama tunavyosoma katika 2 *Wathesalonike 2:8*: *"Ndipo atakapofunuliwa yule mwovu, ambaye Bwana Yesu atamwangamiza kwa pumzi ya kinywa chake, na kumharibu kwa uangavu wa kuja kwake."*

Naam! Na **wanachama wao wote** watakuwa mashahidi wa **anguko la kutisha la mifumo hii ya udanganyifu**, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 14:9–10*: *"Malaika wa tatu akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu akimsujudia yule mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa yake katika kipaji cha uso wake au mkononi mwake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu…"* Mifumo hii ya *"makanisa ya jina tu"* ya **Mpinga Kristo** inajumuisha sehemu mbili, kama tunavyosoma waziwazi katika *Ufunuo 19:20*: *"Mnyama akakamatwa, na nabii wa uongo pamoja naye…"*

Tafsiri ya mafumbo haya ya kibiblia ni:

> *"Mnyama"* = **mfumo wa upapa wa kikatoliki wa kirumi**
>
> *"nabii wa uongo"* = **muungano wa makanisa ya kiprotestanti (ecumenical federation)**




Herufi ndogo **w** inaashiria **kanisa zima likiwa limekamilika na kutukuzwa pamoja na kristo**. Kukamilika huku kwa Mwili wa Kristo na kutukuzwa kikamilifu kwa washiriki wote **144,000** kunatokea **kabla tu ya "wakati wa taabu kuu"**, kama tunavyosoma kwa uwazi katika *Malaki 3:17*: *"Nao watakuwa wangu, asema Bwana wa majeshi, siku ile nitakapowafanya kuwa hazina yangu; nami nitawahurumia, kama vile mtu amhurumiavyo mwanawe mwenye kumtumikia."* Na tena katika *Luka 21:36*: *"Kesheni, basi, kila wakati, mkiomba, mpate kuokoka katika hayo yote yatakayotukia, na kusimama mbele ya Mwana wa Adamu."*

Kanisa hili lililotukuzwa kikamilifu, litakuwa upande wa pili wa pazia **kushuhudia hukumu kuu** juu ya mifumo ya uongo ya kidini, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 14:10*: *"Huyo naye atakunywa katika mvinyo wa ghadhabu ya Mungu iliyomiminwa bila kuchanganywa katika*

*kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele ya Mwana-Kondoo."*

Naam! Kanisa lililotukuzwa kikamilifu, pamoja na Kichwa chake na Mfalme wao – **BWANA YESU – ndilo litalileta kwa mara ya kwanza** hatua **INAYOONEKANA ya Ufalme wa Mungu** katika Israeli, kama ilivyoelezwa kwa mfano katika *Malaki 4:2*: *"Bali kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litatokea, akiwa na kuponya katika mbawa zake…"* Hii ni rejeo kwa **YESU na MWILI WAKE**, wakiwa wametukuzwa kikamilifu, wakijidhihirisha katika mfumo wa **HATUA INAYOONEKANA ya ufalme wa Mungu**.

**x**

Herufi ndogo **x** inaashiria **hatua ya kiroho ya utawala wa ufalme wa kristo au sayuni**. Hii ni **NGUVU, ENZI, na UTAWALA wa serikali ya Ufalme wa Kristo**, kama tunavyosoma katika *Danieli 7:14, 27*: *"Naye alipewa enzi, na heshima, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na mataifa yote, na lugha zote, wamtumikie; enzi yake ni enzi ya milele, haitapita kamwe; na ufalme wake ni wa milele, hautaangamizwa… Na ufalme, na enzi, na ukuu wa ufalme chini ya mbingu zote watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu…"*

Serikali hii ya kiroho ya **Ulimwengu wa Tatu** pia huitwa *"Yerusalemu Mpya"*, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 21:10*: *"Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu."* Naam! *"Sayuni"* itaendelea na **utawala wa kiroho duniani, kwa namna isiyoonekana**, hadi miaka elfu moja itimie mwaka **2874**.

## y

Herufi ndogo **y** inaashiria **kundi kubwa kama watumishi wa sayuni**. Hawa wana **miili ya kiroho (ya kimalaika)** na ni **wa kufa**, na wao ndio watakuwa **watumishi wa kiroho** kati ya hatua ya mbinguni na ya duniani ya ufalme wa Mungu, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 7:15*: *"Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, wakimtumikia mchana na usiku katika hekalu lake; naye aketiye juu ya kile kiti cha enzi atakaa kati yao."* Naam! Hawa ndio **watumishi wa serikali ya kristo katika ngazi ya kiroho**.

## z

Herufi ndogo **z** inaashiria **hatua ya kidunia ya ufalme wa mungu**. Hii inajumuisha **mababu wa imani** waliorejeshwa wakamilifu kama *"wakuu juu ya dunia yote"*, na pia **taifa la israeli lililorejeshwa**, ambao watawaunga mkono katika kazi hiyo kubwa, kama tunavyosoma katika *Zekaria 8:23*: *"Bwana wa majeshi asema hivi, Siku zile itatukia watu kumi, wa lugha zote za mataifa, watamshika mkono mtu mmoja Myahudi, wakisema, Tutakwenda pamoja nanyi, kwa maana tumesikia kwamba Mungu yu pamoja nanyi."*

Wao wataendesha utawala wa ufalme kwa **kutekeleza maagizo ya kanisa**, kama tunavyosoma katika *Isaya 2:3*: *"…kwa maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana kutoka Yerusalemu."* Naam! Taifa hili la Israeli lililorejeshwa linatajwa kama *"jeshi kubwa sana"* katika **unabii wa bonde la mifupa mikavu**, *Ezekieli 37:10*. Hakika, **MATAIFA YOTE**, na pia **vizazi vya waliokufa vinavyorejezwa**,


vitamtafuta Bwana kama tunavyosoma katika *Zaburi 22:27–28*: *"Miisho yote ya dunia watakumbuka na kumgeukia Bwana; na jamaa zote za mataifa watakusanyika mbele zake. Kwa maana Ufalme ni wa Bwana; naye ndiye atawalaye mataifa."*

Naam! Watatamani **kutembea katika utii** wa njia za Mungu kama tunavyosoma katika *Isaya 2:3*: *"…naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake…"* Naam! Hii kazi yenye baraka ya Israeli chini ya **Mababu wa Imani** itakuwa **kamilifu na ya kuridhisha**, kama tunavyosoma katika *Danieli 12:3*: *"…na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele."*

Hii basi ndiyo **Chati katika herufi ndogo – a hadi z**. Sasa hebu tuangalie mwisho wetu kwa kugeukia –

**NAMBA – 1 HADI 11**

Namba hizi zinawakilisha **TAREHE NA MIAKA ILIYOWEKWA**, katika **Mpango Mkuu wa Kimungu**, ambayo Mungu aliikusudia tangu *"kabla ya kuwekwa misingi ya dunia."* Somo hili litatufunulia kwamba **Mungu ni Mungu wa nyakati zilizowekwa na majira**, na mpango wake **hujitokeza inapowadia "utimilifu wa wakati"…** Hebu tuangalie sasa tarehe hizo:




**Namba 1** inawakilisha **Tukio na Wakati Maalum** ambapo **ulimwengu mmoja uliisha** na **ulimwengu mwingine ukaanza**. Hii ni: **siku ambayo gharika ilianza**

Imeandikwa wazi katika *Mwanzo 7:11*: *"Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi…"* Mwaka huu unakokotolewa kama ifuatavyo: **4128 (mwaka wa kuumbwa kwa Adamu) - 1656 (kipindi cha ulimwengu wa kwanza) = 2472 K.K. (mwaka wa kuanza kwa gharika)**

## 2

**Namba 2** inawakilisha **tukio na wakati** unaoashiria: **Mwanzo wa enzi ya wayahudi**

Hii pia ni **mwisho wa Enzi ya Mababu**, mwaka ambao unahesabiwa kuwa ni **mwaka wa kifo cha baba wa mwisho – Yakobo**, na ni mwaka wa: **1812 K.K.**

## 3

**Namba 3** inawakilisha: **Mwaka wa ubatizo wa yesu**

Ilitokea mwaka **29 B.K.**, Yesu alipokuwa na umri wa miaka 30. Tarehe hii inapatikana kupitia **unabii wa majuma 70** katika *Danieli sura ya 9.*

## 4

**Namba 4** inahitaji umakini maalum. Hii inawakilisha: **Tarehe ya kifo cha yesu**, Ilitokea **miaka 3½** baada ya ubatizo wake, katika **Ijumaa, tarehe 3 Aprili, mwaka 33 B.K.**

## 5

**Namba 5** inaashiria tarehe ya: **Mwisho wa majuma sabini ya kibali kwa wayahudi** .Huu pia ni wakati ambapo **mwito wa Injili** ulianza kuwafikia **mataifa**. **Kornelio**, jemadari wa Kirumi na familia yake, walikuwa wa kwanza wa mataifa, kama tunavyosoma katika *Matendo 10:24,44*: *"Hapo kesho yake wakaingia Kaisaria. Naye Kornelio alikuwa amewangojea, akiisha kuwaita jamaa zake na rafiki zake wa karibu… Bado Petro alipokuwa akinena maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno."* Hii ilitokea **miaka 3½** baada ya kifo cha Yesu – yaani:

**Aprili 33 B.K. + 3½ miaka = Oktoba 36 B.K.**

## 6

**Namba 6** inawakilisha: **Tarehe ya kuharibiwa kwa yerusalemu** Hili lilitokea wakati **TITO**, jemadari wa Kirumi, alizingira na kuiangamiza Yerusalemu, kama **utimilifu wa hukumu na unabii** wa *Danieli 9:26*: *"…na baada ya majuma sitini na mawili Masiya atakatiliwa mbali, lakini si kwa ajili yake mwenyewe; na watu wa mkuu atakayekuja wataharibu mji na patakatifu; na mwisho wake utakuwa kama kwa gharika…"* Tukio hili lilitokea mwaka **70 B.K.**

## 7

**Namba 7** inaashiria: **Tarehe ya kurudi mara ya pili kwa bwana wetu,** Hii ilikuwa ni **utimilifu wa unabii wa Danieli 12:12**: *"Heri anayengojea na kufika mpaka siku elfu mia tatu na thelathini na tano."* Naam! Hili ndilo tukio lenye baraka lililotokea mwishoni mwa *siku 1335*. Tukio hili lilitokea mnamo **Oktoba 1874**.

Huu pia ndio **mwanzoni wa Ufalme wa Mungu chini ya Kristo**, ambao utaendelea kwa **miaka 1000**, kutoka **1874 hadi 2874**.

## 8

**Namba 8** inaashiria — tena kwa umakini maalum — **tarehe ya ufufuo wa kwanza wa wale "waliokufa katika Kristo"**, kama tunavyosoma katika *1 Wathesalonike 4:16*: *"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, pamoja na sauti ya malaika mkuu, na pamoja na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza."*

Naam! Hili lilitokea **miaka 3½ BAADA ya kurudi kwa pili kwa Kristo**, kama ilivyofananishwa na kipindi cha kati ya **kuja kwa kwanza kwa Masihi (ubatizo wa Yesu)** hadi **ufufuo wake** kama **Kichwa cha kanisa**, ambacho kilikuwa miaka **3½ baadaye**. Hivyo kwa mwili Wake, tunapata: **Oktoba 1874 + miaka 3½ = Aprili 1878** Naam! Ilikuwa ni katika **siku hii (au tarehe hii)** ambapo **ufufuo wa kwanza ulianza**, na **unaendelea hadi leo.**

# 9

**Namba 9** inaashiria **Tarehe ya ukamilifu wa kanisa**. Hii ni wakati ambapo *Mwili* wa **144,000 utakuwa umetukuzwa kikamilifu!** Hii ni **tarehe ambayo bado iko mbele katika wakati (ya baadaye)**. Je, tutaweza kujua tarehe hii mapema? Jibu linapatikana katika *Amosi 3:7*: *"Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake."* Na tena katika *Isaya 42:9*: *"…na mambo mapya ninatangaza; kabla hayajatokea nawajulisha."* Naam! Uchunguzi wa maandiko haya **unaashiria kwa nguvu** kuwa… **inawezekana**, na kwamba **kanisa litajua kabla ya kutimia kwake!** Tusubiri **Ufunuo wa Bwana katika "wakati ufaao."**

**(TAFADHALI KUMBUKA: Ikiwa kutakuwa na mabadiliko yoyote kwenye chati hii, basi ni katika mstari huu. Inashauriwa kuwa mstari huu unapaswa kuhamishwa karibu zaidi na mstari wa nukta namba 10 katika chati zijazo)**

# 10

**Namba 10** inaashiria **tarehe ya kuanzishwa kwa ufalme unaonekana katika israeli**. Hii inaonyeshwa na **MSTARI WA NUKTA** ambao huashiria **mwisho wa ulimwengu wa pili**, na pia **mwisho wa "wakati wa taabu kuu" na "taabu ya Yakobo"**, kama tunavyosoma katika *Mathayo 24:22*: *"Na kama siku hizo zisingalikatizwa, hakuna mwenye mwili angalioshwa; lakini kwa ajili ya wateule siku hizo zitakatizwa."* Naam! Hii

pia ni **tarehe ya baadaye**, lakini pia kuna **uwezekano** wa kuijua mapema kupitia *Amosi 3:7* na *Isaya 42:9*, kama ilivyoelezwa.

## 11


**Namba 11** inaashiria **tarehe ya mwisho wa ufalme wa milenia**. Naam! Huu ni **mwisho wa miaka 1000** ya Ufalme wa Kristo ambao **ulianza Oktoba 1874**. Hivyo mwaka wa mwisho ni: **1874 + 1000 = 2874 B.K.** Muda mfupi baada ya hapo, **utaanza "muda kidogo"**, kama tunavyosoma katika *Ufunuo 20:7*: *"Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa katika kifungo chake."*

Naam! Huu ndio **wakati wa HUKUMU YA MWISHO na MAJARIBIO** juu ya jamii ya wanadamu waliokamilishwa. Muda huu kidogo utaendelea kwa kipindi kisichojulikana, lakini baada ya hapo, **dunia iliyokamilika yenye wanadamu wakamilifu** itaingia katika **"nyakati za milele"** zijazo.


Naam! Leo tumejifunza **CHATI YA MPANGO WA MUNGU**, inayoangazia **"siku ya saba ya uumbaji"**... Mpango huu wa Kimungu umejengwa juu ya **KWELI KUMI KUU**, kama tunavyoonyeshwa kwa mfano wa *"nyama kumi"* katika *Mwanzo 24:10*: *"Mtumishi akatwa ngamia kumi, wa bwana wake, akaenda…"*

Ah, naam! Kuna **ngamia wengi zaidi**… ndiyo kusema, **kweli nyingi zaidi za mungu** ambazo bado hazijafunuliwa kikamilifu — lakini zitawekwa wazi katika **mpango mkuu wa baadaye wa mungu** kwa ajili ya zile *"nyakati zijazo."*

Ee! **Hakika ni wa ajabu mungu wetu**, na **mwana wake mpendwa** ambaye pia ni **bwana na mwokozi wetu yesu kristo!**


MPANGO WA NYAKATI WA MUNGU
ULIMWENGU WA PILI
ULIMWENGU WA TATU
ULIMWENGU WA KWANZA
KIZAZI CHA WAYAUDI
MAFUNO
KIZAZI CHA INJILI
MAFUNO
UTAWALA WA MIAKA ELFU
NYAKATI ZIJAZO
KARIKA
PATAKATIFU PA PATAKATIFU
PATAKATIFU
ADAMU
ABRAMU
HEMA
YESU
NJIA NYEMBAMBA
KUNDI KUBWA
ISRAELI KUREJESHWA
ULIMWENGU WA MWANADAMU KUINULIWA JUU NA KUFIKIA UKAMILIFU WA UHAI
ISRAELI
NJIA PANA
MAUTI
ULIMWENGU ULIO KATIKA MAUTI NA UKUMU
NJIA KUU
MAUTI YA PILI
"Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomae apate kusoma kama maji."
HABAKUKI 2:2

**AMINA**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***